# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

…Kwa Neno Lako…

Lima, Peru 5–28 Luglio 2017

Mwaka XXII – N. 2, Februari 2020

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


Mhariri

## Maria De Mattias Mlezi

Mwezi wa Pili kwa sisi Waabuduo ni Mwezi wa Mwanzilishi wetu, mwezi wa Mwanamke Shujaa, Mtakatifu, Mama na Rafiki. Mwaka huu kwa namna ya pekee kwenye hafla ya ufunguzi wa Novisiati ya Shirika, tunataka kumtazama yeye kama Mlezi. Tukumbuke kupitia masimulizi ya wale ambao wamemfahamu kwa kina na ambao wana ushuhuda hai wa Utakatifu wake na mafundisho ya maneno yake yaliyokusanywa kutoka barua zake.

Tangu wasichana wa kwanza walipoomba kujiunga na Maria, hamu yake ilikuwa kuwalea Kimisionari wale ambaao walitaka kuwa Waabuduo Damu ya Kristo. Ilikuwa ni Karama ya Shirika la Damu Azizi, ambayo washiriki wake wangetakiwa kuifanya kwa namna ambayo isingeweza kumwagika bure". (Angalia maelezo ya Padre. Michele Colagiovanni)

kwenye Kitabu chake cha kwanza.

Ili kuwa watangazaji wa ujumbe huu, wasichana walipaswa kumpenda Yesu msulibiwa kibinafsi, kwani yeye ndiye pekee aliyeweza kuwasukuma kutoa maisha yao kwa ajili ya wokovu wa roho. Kupitia malezi yake walipata upendo huu na tiba hii. Katika suala hili, katika barua yake moja kwa Merlini, akizungumza juu ya malezi, aliandika: "Wasichana lazima wasaidiwe, watiwe moyo,waonywe kwa Upendo,wasifanye kazi nyingi za nyumbani zinazozidi uwezo wao kwani bado umri wao ni mdogo kati ya miaka 14 au 15. Mabinti hawa maskini wakitunzwa vizuri watakapokuwa watu wazima watakuwa wazuri. Kasoro zao lazima zisamehewe na kurekebishwa kwa upendo na ujasiri; wakabidhiwe mikononi mwa Mama Maria. Kuna ubaya gani katika kufanya hivyo badala ya kusema – Wapelekwe nyumbani -

Kisha nikawaonyesha mifano mingi ya wale ambao niliwarudisha nyumbani,ambao hawakuwa na tabia nzuri (Barua ya 675)




## Muhtasari


*Muhariri*

◇ Maria De Mattias Mlezi 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*

◇ Mkutano wa Mabara Roma 3

*Novisiati maalumu*

◇ Ndoto imetimia 4

◇ Uzoefu wa mpito wa Upustulanti katika Novisiati ya Kimataifa 5

*Toka Ulimwengu wa ASC*

◇ Habari kutoka kwa Grand Cess 8

◇ Sherehe ya Noeli na Watoto maskini toka vijijini 9

◇ Mt. Maria De Mattias, Mwanamke wa kisasa wa Neno 10

◇ Auguri e Ringraziamenti - Albania 11

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*

◇ Furaha kwa Ulimwengu amezaliwa Mkombozi 12

*Katika Shirika*

◇ Kalenda ya Uongozi Mkuu 13

◇ Siku za kuzaliwa : tusherehekee Uhai 13

◇ Waliorudi nyumbani kwa Baba 13



Kwa hiyo haya yalikuwa ni malezi yake ambayo yalilenga ukuaji wa mtu kwa ujumla; katika moja ya barua yake kwa Sista Maria Giuseppa Flavoni, ambaye alikuwa amekabidhiwa msichana aitwaye Maria Filomena huko Sodezza na Saviezza, alisema kadiri ya mtazamo wake kwamba; alikuwa hodari katika kazi ya ushonaji, uandishi na katika mahesabu.(.....) na kwa usafi, na utanashati wa mavazi. (Lit. 425).

Mara nyingi sana mapokezi ya wasichana yalikuwa sababu ya msalaba, sababu ya mateso na migogoro katika jumuiya, lakini alijua kwamba malezi pia ni kazi ya Roho na Neema na ndivyo alivyoamin: "Niliwapokea wasichana hao kwa moyo wangu wote na wala sikwenda kuwatafuta, na kwa machozi ya huruma niliwaweka mikononi mwa Maria Mtakatifu, ili aweze kuwalinda na kuwatetea, kwa kuwa hawawezi; na sasa oh! (Barua.631)

Maria alikuwa akifundisha kwa mifano; na hapa anatolea mfano wa Mama Clementina Zerr na Sista Paolina Feser wanathibitisha hili waliporudi kutoka Ujerumani, walikuja kukutana na Maria De Mattias. Licha ya ugumu wa lugha, hiki hakikuwa kikwazo. Watawa wawili vijana wa Ujerumani, ambao wangekuwa Waabudu wawili wakubwa, waliguswa na ushuhuda wake wa maisha, na Roho yake ya sala, walimshukuru sana kwa ile shauku ya kupenda kusulubiwa, ambayo ilimpelekea kumpenda "jirani mpendwa" na kwa moto kama huo ambao ulimpelekea Yesu kufa msalabani.

Nia ya Mwanzilishi wetu ilikuwa kuwafanya wasichana hawa wampende Yesu, na wawe na shauku ya Kimisionari kwa ajili ya wokovu wa roho.Karama ambayo Roho amempa Mwanzilishi hubeba ndani yake nguvu inayopita wakati na nafasi. Ndiyo maana mbele yetu kumefunguliwa malezi ya Novisiati ya Shirika: hamu ya kupata njia za kujieleza na kujimwilisha katika historia ya leo na ukweli wa kitamaduni.

***Sr Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Mkutano wa Umoja wa UISG Roma

Mada: "Mbegu za tumaini la kinabii ... zinazalisha mienendo ya KITAMADUNI"
Roma, 9 na 10 Januari 2020,

Huko Monte Cucco, Mnamo tarehe 10 Januari 2020, wakati wa Mkutano wa kila mwaka wa Wakuu wa Mashirika mbali mbali wanaoishi Roma, Sista Nadia Coppa Mwabudu wa Damu ya Kristo, alichaguliwa kuwa mjumbe wa UISG kwa Mashirika ya Kimataifa yaliyoko Roma, Tunampongeza, na kumtakia kila la Heri Sr. Nadia katika kulihudumia Kanisa la Mungu. Tunawashukuru kwa kukubali kazi hii, ambayo kama Waabuduo Damu ya Kristo, bi harusi wa Mwanakondoo wa Pasaka, inatufungua zaidi na zaidi katika kushiriki na kuimarisha utambulisho wetu kama wanawake waliowekwa wakfu katika Kanisa, kukubali changamoto zinazojitokeza leo katika Mashirika yote.






ROME CONSTELLATION MEETING ROME CONSTELLATION MEETING



Auguri
Suor Nadia

# Ndoto imetimia

*Februari 4, 2020, ni Sikukuu ya Mtakatifu Maria De Mattias na siku ya kuanza kwa Novisiati ya Shirika*

Historia.

Mkutano Mkuu wa 2017 ulifanikiwa kutimiza kile ambacho kwa muda mrefu kimekuwa ni hamu ya pamoja ya Shirika zima: kuwa na Novisiati Moja (ya Shirika zima). Kusudi la msingi la chaguo hili ni kusaidiana ili tuweze kukua kama mwili mmoja, kuushinda mgawanyiko na kuweka nguvu pamoja.

Hii ni ndoto ambayo utambuzi wake umekabidhiwa na hati za Mkutano Mkuu, kwa Uongozi mpya. Mradi huo ulihamasishwa na maono ya kuunda ASC mpya, yenye wanawake ambao, wametiwa mbolea ya Neno la Mungu, ili wamzae Kristo na kuleta upendo wake katika ukweli wa wakati wetu; wanawake wanaofanya mazungumzo kwa pamoja, watawezeshwa kugundua uwepo wa Mungu, mbegu ya tumaini, na uzima mpya.

kwamba kila mmoja abebe ndani yake mwenyewe; wanawake wenye uwezo wa kuhusiana na watu na tamaduni tofauti,na kujisikia nyumbani kila mahali watakapokuwa, kwa sababu Region zao za asili ni Jumuiya ya ASC na mahali pa utume wao ni ufalme wa MUNGU. Mabadiliko haya makubwa katika michakato ya malezi yatatusaidia kupyaisha Karama ya ASC katika mazingira ya kihistoria na kitamaduni katika mabadiliko yanayoendelea.

Ili kutoa uhai kwa mpango huu, ilikuwa ni lazima kuunda mazingira ya kitamaduni kulingana na Jumuiya ya Waabuduo kutoka asili na tamaduni tofauti.

Uongozi Mkuu ulitoa kipaumbele kwa mpango huo. Kupitia sala na utafiti, waligundua mahali, kisha watu wenye uwezo wa kujenga Jumuiya mpya ya malezi na, hatimaye, Washauri Wakuu ambao wangeandamana nao.

Masista walioteuliwa kuunda Jumuiya hii ni:

Sr Mariamma Kunnackal, mwalimu Mkuu wa Wanovisi, na Makamu wake Sr John Stoverink, Sr.Emanuela Škarica, alikubali jukumu la mkubwa wa Jumuiya; Sr Marisa Nardoni alichaguliwa kuwa muhasibu wa jumuiya, na Sr Martha NKwimba, kama mwanajumuiya kijana wa Jumuiya ya malezi. Masista hawa waliwasili Roma mnamo Septemba, 2018, katika Nyumba Kuu ili kupata uzoefu wa Jumuiya ya kimataifa na kuwa tayari kwa malezi ya Jumuiya ya kitamaduni, kukabiliana na wito wa mabadiliko, kwa ndoto ya ASC, katika kujenga sasa ule utaratibu mzuri wa vitu.

Kwa kuongezea, washiriki wa Jumuiya ya Malezi walisomea kozi za mambo ya kiroho kila mwezi, walishiriki kulingana na hali halisi ya ukweli mwingine wa Shirika juu ya hali ya Roho ya ASC. Haya waliyapata kutoka kwa Masista wa sehemu mbali mbali za Ulimwengu kwa njia ya Skype. Utaratibu huo ulihusisha vyombo vyote, kuanzia vikubwa hadi vidogo, na kumpa kila mmoja fursa ya kutoa mchango wake na uzoefu wake. Kwa njia hii, Masista waliweza kujilinganisha na Mashirika mengine ya Kimataifa, ambayo yalifanya uchaguzi ule ule wa malezi na wako katika hatua ya mbele zaidi.

Kwa sasa Tume iliyoundwa na washauri ambao ni Sr Wieslawa Przybylo, Sr Matija Pavić, Sr Mariamma Kunnackal, Sr Maria Hughes na Sr Joan Stoverink, wamefanya kazi katika maendeleo ya mpango wa malezi, ambao ulihusisha Shirika lote kupitia usambazaji wa maswali. CGE, ambayo ilifanyika Roma mnamo Novemba, 2018, pia iliupatia Uongozi Mkuu na Wakuu wa Region fursa ya kujadili michakato inayoendelea ya utayarishaji wa Novisiati ya Shirika na kusikiliza uzoefu wa Jumuiya nyingine za kimataifa, ambao tayari wako katika hatua ya uchaguzi huu.

Kwa hiyo, mnamo Septemba 4, 2019 akina Masista wa Jumuiya ya malezi ya Shirika, walihamia kwenye nyumba iliyochaguliwa kama Makao ya Novisiati, G. Gatti, 13 huko Roma. Nyumba hiyo, inayomilikiwa na Region ya Italia, hapo zamani ilikuwa makao ya Novisiati katika miaka ya 1980 - 1990, iliyouzwa kwa mkopo kwa ajili ya matumizi ya utume huu wa Uongozi Mkuu, imekarabatiwa tena kwa ajili ya Jumuiya ya malezi. Mnamo Novemba, waanzilishi saba wa kwanza wa Novisiati ya Shirika kutoka maeneo tofauti walifika Roma.

***Sr Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

# Uzoefu wa kipindi cha mpito cha Upostulanti katika Novisiati ya Shirika







Kufika kwa Wapostulanti saba kulikamilika mnamo 18 Novemba, 2019. Nyumba hiyo ilijaa furaha na vicheko kwani wasichana walikuwa wamekutana kwa mara ya kwanza. Kwa kipindi hiki cha miezi miwili ya mpito, wasichana wamekuwa wakifanya kazi kwa kufahamiana zaidi, kukuza lugha ya Kiingereza, na kujifunza kuthamini tamaduni tofauti.

Wakati Sista Joan Stoverink alipokuwa akifundisha Kiingereza nyumbani, tulijitahidi kutumia lugha ile ile kama njia ya mawasiliano ili kujifunza vyema; kwa kuwa tupo nchini Italia tumeona kwamba kuna umuhimu wa kujifunza lugha ya Kiitaliano. Ili kurahisisha mawasiliano na watu wa Parokia hiyo pamoja na majirani,lakini pia ili kutekeleza huduma ya uhamasishaji na pia kuwasiliana na Waabuduo wanaokuja kututembelea na hawajui kiingereza. Sista Enrica Cinti, ASC amekuwa akifundisha maneno kadhaa ya msingi ya lugha ya kiitaliano.

Ili kufahamiana zaidi tumekuwa tukitoka na kwenda sehemu mbalimbali. Na wakati wa kipindi cha Majilio tumeshiriki siku nzima katika kutafakari juu ya Liturjia ya wakati huu na Masista waingereza na waandishi wa habari huko Nyumba Kuu ya Shirika.

Tumewatembelea Masista wa Shule ya Mama yetu wa Dame (SSND) ; tulitembelea Makanisa Makuu manne ya Roma na makanisa mengine ili kuangalia mapango ya Noeli, tulitoa chakula kwa maskini na tukahudhuria tamasha la Krismasi, mnamo Desemba 22, Katika nyumba Kuu; Kwa namna ya pekee tulishiriki katika Ibada ya kichungaji na Papa Fransis. Tukio lenye kutajirisha zaidi lilithibitika kwenye mkutano wa Jumuiya wakati ambapo tulishirikishana juu ya utamaduni wetu na historia ya miito yetu ambavyo vilitusaidia kufahamiana zaidi. Baada ya kushirikishana, wakati wa jioni zilifuata nyimbo na michezo ya tamaduni mbalimbali.

Kila wiki huwa tunakutana na wapostulanti mmoja mmoja, vile vile huwa tunasali masifu ya asubuhi na, wakati mwingine huwa tunatafakari Neno la Mungu na kuabudu Ekaristi Takatifu. Kwa siku zilizofuata Wanovisi watarajiwa wamekuwa wakipata vipindi vya masomo ya Bibliodrama, ambayo ni namna tofauti ya kukaribisha Neno la Mungu; mnamo Januari walihudhuria masomo ya Teologia ya Nadhiri, masomo ya Saikolojia na masomo ya mienendo ya vikundi.

Huwa tunashiriki Ekaristi Takatifu kwa lugha ya Kiitaliano katika Parokia ya Mtakatifu Agnes na mara mbili kwa wiki huwa tunaenda kwa miguu kwenye kanisa la Masista wa Ursuline kushiriki Ekaristi kwa lugha ya Kiingereza.

Wapostulanti wanaonekana kufurahiana wao kwa wao na wanafurahi na kila mmoja, wanasaidiana, pia wanasali na wanakula pia kila aina ya chakula. Tunamwomba Bwana awabariki kwa uweza wake na awape neema ya kukabiliana na mshtuko na changamoto zote za kitamaduni na awajalie amani na utulivu. Wanajumuiya wote wa Jumuiya ya malezi ni msaada muhimu kwao. Kwa hisia hizi tunaendelea na safari tukiwa na moyo wa shukrani na furaha. Tunaushukuru Uongozi Mkuu kwa ukaribu na msaada wao.

***Sr Mariamma Kunnackal, ASC***
***na Sr JoanStoverink, ASC***



Ninaitwa ***Suchitra Paik***, nina umri wa miaka 20.
Natoka Jimbo la ODISHA. Ni mmojawapo wa Region ya India
Kwa sasa ni Mpostulanti , na hivi karibuni nitakuwa Mnovisi
Kwa mara ya kwanza nilikutana na Masista walipokuwa wakihamasisha miito
katika uwanja wa ufundi na kupitia kwao nilikutana na Mtakatifu Maria De Mattias.
Maisha yake ya unyenyekevu yaligusa moyo wangu.



Ninaitwa ***PadmaVaddeaswarapu***, nina umri wa miaka 20.
Natokea Jimbo la Andra Pradesh.
Ni mmojawapo wa Region ya India.
Kwa sasa ni mpostulanti.
Kwa mara ya kwanza nilikutana na Masista walipokuwa wakihamasisha miito,
na kupitia kwao, nilikutana na Mtakatifu Maria De Mattias.
Nilivutiwa sana na bidii yake.




Naitwa ***Martina Bukarica***, Nina umri wa miaka 29.
Natoka Croazia. Na ni mmojawapo wa Region ya Zagabria.
Kwa mara ya kwanza nilikutana na Sista wa Shirika letu huko Zara ambaye namna yake ya kuishi ilinivutia sana.
Kwa kupitia kwake niliweza kumfahamu Mtakatifu Maria De Mattias.
Napenda jinsi Mtakatifu Maria De Mattias alivyokuwa na Upendo kwa Damu ya thamani ya Kristo.




Naitwa ***Swarnalatha Bandi***, nina umri wa miaka 20.
Natoka India, Jimbo la Andra Pradesh.
Ni mmojawapo wa Region ya India, na sasa ni Mpostulanti
Kilichonivuta ni maisha ya Masista ASC wa Parokia yangu ya Velgode, mahali ambapo nilimfahamu Mtakatifu Maria De Mattias



Naitwa ***Biljana Kostić***, nina umri wa miaka 20
Natoka Banja Luka iliyoko Bosnia Erzegovina.
Ni mpostulanti wa ASC na ni mmojawapo wa Region ya Zagabria. Niliwafahamu ASC tangu kuzaliwa kwangu; nilisoma katika Parokia waliyokuwepo.
Kupitia Masista hawa, nimemfahamu mwanamke Mkubwa, grande donna, dada na Mtakatifu, Mpendwa Maria De Mattias.



Naitwa ***Mary Priya***, umri wangu ni miaka 22.
Natoka Karnataka na ni mmojawapo wa Region ya India. Ni mpostulanti.
Nimewafahamu ASC tangu nikiwa kijana mdogo. Nimesoma katika shule yao, na kupitia kwao nimemfahamu Mtakatifu Maria De Mattias. Kilichonivutia ni Upendo kwa Yesu Msulibiwa.



Naitwa ***Romina Giacconi***, nina umri wa miaka 45.
Kwa asili natokea Agugliano katika Mkoa wa Ancona
Ni mpostulanti wa Region ya Italia; mnamo mwaka 2013 nilikutana na Waabuduo
Wakati wa mkutano juu ya huruma uliofanyika katika mji wangu na Sr. AnnaMaria Vissani asc.
Ili kuandika kile ambacho kilinigusa zaidi juu ya Mwanzilishi wetu Mtakatifu Maria De Mattias, nachukua sehemu ya maneno ya Padre Yohane Merlini: Per descrivere ciò che più mi ha colpito della fondatrice Santa Maria de Mattias: "Mwanamke hodari, jasiri na mcha Mungu."

## *"Tuko wamoja katika Roho, sisi ni wamoja katika Bwana."*

Sisi, Wapostulanti saba (hivi karibuni tutakuwa Wanovisi) kutoka Region tofauti za Shirika. Tulikuja Roma kuanza uzoefu mpya wa ASC: uzoefu wa kitamaduni. Tunamshukuru Mungu kwa kutupatia fursa hii ya kuishi pamoja kutoka tamaduni tofauti. Kumwona Papa na kusali karibu na mwili wa Mtakatifu Maria De Mattias ilikuwa ni tukio la kipekee na la muhimu kwetu.
Maisha yetu ya kila siku yamejaa furaha na kicheko. Wakati mwingine kuna ugumu wa kuelewa lugha, lakini hii haileti kikwazo katika mahusiano yetu. Tuko hapa kila mmoja kwa ajili ya mwingine, tayari ku saidiana katika hali yoyote. Masista wa Jumuiya yetu wanatufanya tujisikie nyumbani. Tunafurahi kukua katika Novisiati hii ya kitamaduni na tunawaomba mtusindikize kwa sala zenu za thamani. Nasi pia tunaahidi kuwakumbuka katika sala zetu.

Eneo la Bara: Africa
Misheni Liberia

# Habari kutoka Gran Cess

*Masista kutoka Liberia wanatusimulia jinsi walivyosherehekea Krismasi yao.*

Hakika Mwezi Desemba ulikuwa ni mwezi wenye utajiri wa matukio. Mbali na ujio wa Krismasi, mnamo Desemba 29 tulisherehekea Upadrisho wa Padre Andrew Toe ambaye asili yake ni kutoka Gran Cess, hii iliambatana na Misa ya Shukrani; chakula cha mchana kiliandaliwa kwenye bustani iliyoko mbele ya kanisa (chakula hiki kiliandaliwa katika jiko letu. Wakati wa mchana tulikuwa tukiangalia michezo ya asili kutoka vikundi mbali ambavyo viliwafurahisha sana watazamaji. Katika hafla hiyo, tuliwakaribisha Masista sita wa Shirika la Familia Takatifu ambao walilala kwa siku mbili. Masista hawa walikuja na magodoro yao kwani kulikuwa na vitanda viwili tu ndani ya nyumba yetu. Hivyo walilalia magodoro yao.






Mnamo Desemba 22, ilipangwa kuwaambia rasmi wanaparokia kuhusu kuondoka kwetu mwezi wa Februari. Mungu ana njia zake ... na tarehe ya tangazo iliahirishwa hadi Januari 5, ninaelezea hapo chini kwanini:

marafiki wa Sista Zita walilipa ada kwa mtu ili aitumie kwa mwaka katika shule ya kitaalam ya Harper akasomee mambo ya umeme, ni umbali wa masaa matatu, na Desemba 21, kwenye hafla ya utoaji wa diploma, aliamua kuwashangaza kwa kwenda kwenye sherehe pamoja na mke wake na watoto wake wawili. Baba Francis alikuwa ameambiwa kwamba barabara zilikuwa katika hali nzuri ukilinganisha na msimu wa mvua na hivyo alijitolea kukiendesha kikundi hicho, ilikuwa siku nzima ya kusafiri.

Kwa ufupi ni kwamba: wakiwa safarini walikwama kwenye matope mara tatu na ikabidi walikwamue gari kwa kuchimba, walipokwama kwa mara ya mwisho ilikuwa ni saa nane za usiku wa giza nene, katikati ya msitu, betri ya gari ilikuwa chini kwa sababu ya sehemu iliyovunjika ya mbadala. Sista Zita na watoto wawili pamoja na mama yao, walifika kwa baiskeli saa 4.00 Asubuhi Jumapili ya tarehe 22 na tangazo lile halikutangazwa Kanisani. Walakini gari lilirekebishwa na kufikishwa jioni ya Siku ya Krismasi, Baba Francis ni fundi mzuri na ilikuwa uthibitisho kwamba alikuwepo kwa kipindi kile kigumu. Tumshukuru Mungu kila kitu kilienda vizuri.



Jioni ya Desemba 24, baada ya Misa ya saa 5.00 Usiku, Mapadri walijiunga nasi kwa chakula cha jioni ambacho kilikuwa ni tambi, nyama za kuku, njegere na keki. Zawadi tuliyopeana ilikuwa ni chupa ya divai ambayo tulikuwa tumetenga kando kwa ajili ya siku hii!

Mwishowe, katika ua wa parokia ambao upo kwenye nyumba yetu, kisima kipya kinachimbwa pamoja na kazi nyingine nyingi, NGO ya Ujerumani inafadhili mradi huu, labda kati ya $ 15,000 na $ 20,000 ya vifaa na kazi. Chemchemi hii siyo tu baraka kwetu, lakini pia kwa shule hiyo kwa kuwa zaidi itakuwa chanzo cha maji mazuri wakati ambao kisima cha shule kitakuwa kikavu. Basi NGO itarudi mnamo 2020 kujenga kisima kipya kwa ajili ya hospitali.

*Nawatakia heri ya mwaka mpya kwa wote.*

***Sr Therese Wetta, ASC***

# Sherehe ya Noeli na watoto maskini toka Vijijini

*ASC wa India ambao hufanya kazi shuleni katika maeneo tofauti wametusimulia jinsi walivyosherehekea Krismasi pamoja na watoto.*

## *Kaskazini mwa India Karnataka – Tarikere*

Krismasi ilikuwa ni wakati wa furaha kwa watoto wote ambao walikuja pamoja kusherehekea.

Watoto 55 kutoka vijiji 3 vya Tarikere Taluk walikuwepo. Saa 5.30 Usiku tulianza na mpango wa sala iliyoandaliwa kwa njia ya kucheza na kila kijiji kiliwasilisha mpango wake wa kitamaduni ambao ulikuwa mzuri. Washiriki, walijipanga kimadarasa na kulingana na umri wao, walishindana katika mashindano ya michezo na washindi walipewa tuzo za kupendeza. Padre wetu wa Parokia hiyo P. Ealise alitoa ujumbe mfupi wa Krismasi na saa 8.30 mchana alifunga sherehe hiyo kwa chakula cha mchana.

**_Sr Rotion Mangarayil , ASC_**





## *Kaskazini mwa India - Jharkhand - Ranchi*







**_Sr Jancy Pallicka, ASC_**

## *Karnataka - Mysuru*
## *Kengele za Krismasi zinalia na kumfanya kila mtu aimbe!*






Sherehe ya Krismasi ilianza kwa sala na wimbo pamoja na taa ambayo ilikuwa imewashwa ikiashiria kwamba Yesu ni taa ya Ulimwengu. Hafla hiyo ilihudhuriwa na (Vikundi vya Msaada wa ShG) na vijana kutoka kozi ya mafunzo kwa walimu wa chekechea (NTT - Wanafunzi wa Mafunzo ya Waalimu wa Nursery) ambao walicheza vizuri. Ulifika wakati wa kukata keki, maana bila keki Krismas ingekuwa haijakamilika. Mkurugenzi wetu Sr Jaisy alitutakia Krismasi Njema. Wanafunzi wa NTT waliimba nyimbo za Krismasi, na hatimaye zawadi zilisambazwa kwa washindi wa michezo.

**_Sr Jaicy Karukuttikaran, ASC_**

# Mtakatifu Maria De Mattias, Mwanamke wa sasa wa Neno

Tukiangalia na kutafakari kwa kina juu ya maisha na barua za Mtakatifu Maria tunaweza kuona kweli kwamba aliishi maisha ya kiinjili na kanuni za msingi za kikristo. Kwa kweli, Maria alikuwa mwanamke wa kanisa ambalo Maandiko Matakatifu hayangekuwa ni kitu ambacho kinapaswa kutengwa na maisha, kitu kisichoweza kufahamika, bali yalikuwa ni sehemu muhimu ya maisha yake ambayo yalichochea na kuonyesha mtindo wake wa maisha.

Kwa hivyo, tunaona kuwa Roho Mtakatifu alimwongoza kuchagua roho ambayo ni moyo wa Kanisa na pia moyo wa Yesu Kristo, ambayo ni, Roho ya Damu ya Kristo.

Tunaweza kudhibitisha kuwa Maria De Mattias alikuwa mwanamke wa "NENO" haswa kwa sababu aliishi katika mada kuu ambazo Agano Jipya linapendekeza na kuelezea; "Rehema ya Kimungu na Neema ya Mungu". Injili za Synoptic, haswa simulizi la Luka, ambalo linaangazia hali ya huruma ya Mungu katika mifano ya baba mwenye rehema, (Lk 15, 11-32), ya Msamaria mwema, (Lk 10, 25-37) ya kondoo aliyepotea, (Lc 15, 4-7), pesa iliyopotea (Lk 15, 8-10) na historia ya Zakeo (Lk 19, 1-10), nk. Yesu anaonyesha huruma kubwa ya Mungu mbele ya masikitiko ya dhambi ya aibu ya mwanadamu. Hii haipo kabisa kwa sura ya Mungu wa Agano la Kale: Mungu mwenye adhabu ya kutisha, bali Ufunuo wa Yesu juu ya Baba yake kama Mungu anayesamehe, na ambaye hutubadilisha na kutufanya kuwa warithi wa Yesu na wa utukufu wake mwenyewe (Ebr 9, 15-16).

Tafakari ya kina ya barua za kiroho za Mtakatifu Maria bila shaka ilifunua hali nzuri ya moyo wake. Sehemu kubwa ya barua zake inaonyesha kwamba anamtegemea Mungu na Rehema zake. Zaidi ya hayo, barua zake zinashuhudia kwamba mara nyingi alikuwa akimtegemea Mungu. Akichochewa na unyenyekevu mkubwa na roho ya kujitiisha, anakiri mapungufu yake na udhaifu wake. Maria De Mattias akiiamini huruma ya Mungu, aliweza kuiona katika maisha yake yote. Ulinganisho wa maisha yake na Neno la Mungu umesaidia kujigundua, kuishi kwa uangalifu, kila wakati sasa na sio wakati uliopota. Ujuzi kamili na uthabiti wa hisia na mawazo vilimsaidia Maria De Mattias kuuchonga utu wake na kufikia kilele cha ukomavu wa kibinadamu na kiroho. Hii ni kwa sababu maishani mwake amewahi kuona utimilifu wa huruma ya Mungu. Bila kizuizi, Maria alijitambua kama mtumishi mnyenyekevu wa Mungu na barua zake zote zinatoa taswira dhahiri ya ubora huu wa kipekee.

"Kwa utimilifu wake wote tumepokea: neema juu ya neema." (Jn 1, 16-17). Yohana anafafanua katika Injili yake kwamba sote tumepokea neema juu ya neema. Ikiwa ni kwa rehema za Kimungu kwamba tumesamehewa ni sawa na neema na kulingana na kipimo cha imani yetu tunakombolewa. Mtakatifu Maria De Mattias alikuwa mfaidika wa neema ya Mungu ambayo ilimwezesha kukaa masaa mengi katika kutafakari juu ya Bwana aliyesulubiwa. Imani yake ilikuwa ya ajabu na kwa hivyo mto wa Neema ulitiririka kupitia maisha yake! "Neema yangu inakutosha, kwa sababu nguvu zangu zinajidhihirisha kamili katika udhaifu" (2 Kor 12: 9-10) Yesu anasisitiza na kumtia moyo mtakatifu Paulo avumilie katika wito wake.

Kwa sisi Waabudu, katika Mkutano Mkuu wa 21 lengo lake lilikuwa ni kusikiliza Neno kila siku na kuliingiza katika mchakato wa mabadiliko ya kibinafsi. Sisi pia nchini India tumechagua mada ya "jamii iliyojikita katika Neno" ambayo kimsingi inaturudisha kwa Mtakatifu Maria, ambaye aliishi maisha yake kwa ukamilifu kulingana na Neno. Maisha yake na hali yake ya kiroho inakuwa chanzo cha kuaminika na kinachofaa kwetu hata leo, ikitupatia changamoto ya kupata uhai katika Maandiko Matakatifu. Kuishi kwa uthabiti na Neno ni kupata ujuzi wa neema na utimilifu wa huruma ya Mungu kwetu na ndani yetu.

***Sr Beena Thoombalan, ASC***

Eneo la Bara: Ulaya
Misheni ya Albania

# Heri na Shukrani

*Katika hafla ya Krismasi, Sr Suela Pepa, ASC Mkubwa wa nyumba ya Durres - Mamurras - Albania, iliyokumbwa na tetemeko la ardhi la Novemba 26, aliwashukuru kila mmoja kwa mshikamano waliouonyesha.*

**«Msiogope : kwa kuwa, mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuuitakayokuwa kwa watu wote: leo, katika mji wa Daudi, amezaliwa kwa ajili yenu, ndiye Kristo Bwana.**
**Na hii ndiyo ishara kwenu: mtamkuta mtoto mchanga, amelala katika hori ya kulia ng'ombe».**

**Lc 2,13**

Wapendwa,

tunaposherehekea Krismasi, Mungu anaingia katika historia yetu, anachukua udhaifu wetu na anakuja kutukuta katika udogo wa mtoto mchanga. Ninapofikiria juu ya Krismasi hii ya 2019, kinachoendelea katika akili yangu ni kilio cha mtoto anayekuja, ni kilio cha Uhai.

Pia ni Krismasi ya huko Durres na Mamurras, maeneo ambayo yalikumbwa na tetemeko la ardhi. Kila asubuhi nilipokuwa nikipita mbele ya jengo hilo lenye vyumba sita vilivyoanguka karibu na nyumba yetu, ambapo watu saba walipoteza maisha katika usiku wa giza, ni kama nilikuwa nasikia bado kilio cha mtoto huyo chini ya kifusi ambaye alikuwa na hali mbaya.

Nilipokuwa nikitembea katika ua wa Durres, maneno ya mtoto Ledion kidogo yalinishangaza na yaliitetemesha Dunia, kwa machozi na kwa sauti iliyokuwa ikipiga kelele "Mungu utusaidie", na mtoto mdogo alikuwa akicheza chini na mdoli wake kwenye matope ya Thumana, kunyamaza kimya kwa maumivu ya yule ambaye kutoka umaskini alikuwa ameshakuwa maskini.

Katika mitaa ya jiji na kuta za majengo yaliyoanguka, naona watoto ambao wamepoteza tabasamu, nyumba za familia zao.

Katika macho yangu anarudi Ajsel mdogo, akiwa kwenye kitanda chake chekundu kwenye ua wa kanisa hilo, ambalo, bila kujua, alilala juani wakati katika kitongoji kingine, kati ya magofu, maisha yalikuwa yamezimika na watu walio karibu naye walikuwa wamejaa uchungu.

Ishara kwetu, mtoto amevikwa nguo za kitani!

Ndiyo! Mungu huja kututembelea katika maisha yetu ya kila siku, tunapokuwa hatuna utulivu, usalama wetu uliporomoka kwa huruma na uaminifu wa mtoto. Ni Krismasi! Mtoto alijifunga na kuwekwa ndani ya chombo cha kulishia ng'ombe, Emanueli, "Mungu aliye pamoja nasi, anaingia katika historia yetu" anasimama karibu na wanawake na wanaume wa nchi yetu, katika wakati huu wenye uharibifu na woga, kurejesha kizazi cha maisha mpya, pia kupitia wale ambao kwa ishara halisi hutusaidia kuinuka na sio kuangalia giza bali nuru.

Matumaini yetu ni kwamba upendo, huruma na busara ya Mungu, viguse kila moyo uliogawanyika, kila jeraha lifungwe, kila mgonjwa aponywe, kausha machozi yetu, tuwe na hakika kwamba wewe u pamoja nasi na kamwe hutatuacha.

Tuwe na matumaini na uhakika kwamba hakuna tetemeko la ardhi na hakuna kifusi kinachoweza kuporomosha upendo ambao Mungu anatujalia.

Tunawatakia kila la kheri ninyi, ambao kwa ukarimu wenu na msaada wenu mmepanua hema la mioyo yenu kwa kuwakaribisha na kuwapa mahali pa kukaa wale ambao hawana makazi.

Tunawashukuru kwa dhati kwa yote ambayo mmeyafanya na mnaendelea kututendea, kwa ardhi yetu na watu wetu.

*Emanueli, Mungu wa amani, awape furaha na utulivu ninyi na familia zenu.*

***Jumuiya ya ASC huko Albania, Durres - Mamurras.***
***Sr Suela Pepa, ASC***



# Furaha kwa ulimwengu, Mwokozi kazaliwa!

Malaika waliimba: "Utukufu kwa Mungu mbinguni na amani duniani, aleluya! Tangazo hili linawaamsha wachungaji na Wafalme, ili wamwone mtoto Yesu katika chombo cha kulishia ng'ombe na kutafiti Upendo wa Mungu katika fumbo kubwa la kujimwilisha. Tutafakari unyenyekevu wa Mungu ambaye alijifanya mtu kwa kukutana na kila mwanamume na mwanamke.

Krismasi ni wakati wa kugawana furaha yetu, ya Upendo na wakati wa kufanya upya uhusiano wetu. Furaha ni ile ya Yesu Mwokozi aliyekuja kati yetu kutuokoa kutoka kwa sanamu zetu zote za ulimwengu na kutufahamisha kuwa Mungu ni Upendo. Kwa sababu Baba alitufanya kuwa zawadi ya Mwana, kwa hivyo Krismasi ni wakati wa ubora wa "zawadi" Sisi pia tumeitwa tujifanye zawadi ya ukarimu wa Mungu Baba kwa kushiriki maisha yetu na jirani zetu.

Usiku wa Krismasi ni wakati wa neema tu kwa wale ambao wako tayari kuipokea, kwa wale wanaotaka uhuru na wokovu mioyoni mwao. Lakini tunapoangalia ulimwengu, bado kuna vita na uharibifu, watu wasio na hatia ambao wanakufa, watoto ambao wananyanyaswa na kuharibiwa kijinsia, na watu wote ambao wanakufa na njaa kwa sababu ya majivuno na ubinafsi wa wenye nguvu, watu wengi hawapendani. Hii inachangiwa na chuki, wengi wanaishi bila tumaini nk. Injili ya Lk 4,18-19 inatuambia: "Yesu alikuja ulimwenguni kuleta habari njema kwa maskini, kutangaza uhuru kwa wafungwa, na kuwainua waliokandamizwa ...".

Krismasi hii ya 2019 ilikuwa maalum sana na muhimu kwangu na kwa sisi sote katika Jumuiya ya Nyumba Kuu. Kwa kweli, tunatoa shukrani kwa Jumuiya ya Mtakatifua Egidio, tulipata nafasi ya kufungua milango ya mioyo yetu na nyumba kwa maskini, wapweke, waliotengwa na watu walio katika mazingira magumu. Kwa kweli mnamo Desemba 25 tulisherehekea Krismasi na wakimbizi, wahamiaji na watu wasio na makazi. Waliohudhuria Sherehe hiyo walikuwa karibu watu wazima 150 na watoto. Kwa kuongezea, waliandaa pia adhimisho la Ekaristi. Si hilo tu, bali waliandaa na kugawa chakula cha mchana cha Krismasi pamoja na kuimba nyimbo za Krismasi. Na hatimaye waligawa zawadi binafsi kwa kila mtu.

Wageni wetu walifurahi sana. Sisi Masista waabuduo Damu ya Kristo tulikaa mezani pamoja nao kula chakula cha mchana lakini pia na zaidi ya yote, furaha ya kujisikia wamoja, ya kutazamana kwa macho kujitambua kama watoto wa Mungu na kaka na dada kati yetu. Kwa kweli, baada ya kumkaribisha Yesu katika nyuso zao, mabadiliko kamili yalifanyika katika mtazamo wetu, Upendo wa ukarimu ambao hutoa furaha ya ndani na maelewano kwa kuwa pamoja, kusikiliza shida zao na kujifunza kuwafahamu watu namna hiyo zaidi ya ubaguzi wa kawaida. Wakati Jumuiya ilipokutana mezani kwa chakula cha jioni, kila mmoja alishirikisha furaha yake.

Pamoja na hawa ndugu zetu waliojeruhiwa na wanaoteseka Na hawa ndugu na dada zetu waliojeruhiwa na wanaoteseka,tumechochewa na kutiwa moyo wa kuwa na huruma tukiahidi kumwomba Mungu Baba ili aweze kuufanya ulimwengu uwe wenye haki zaidi.



Mnamo Desemba 29, Jumuiya ya kimataifa ilitembelea Masista wazee wa Nyumba ya Betania, huko Roma. Tuliweza kutumia masaa machache nao kushiriki furaha na upendo wa Krismasi ambayo tuliipata. Pamoja nao tulicheza bingo na kusambaza zawadi kwa washindi, na zaidi pia kulikuwa na tuzo za faraja, tukaimba nyimbo za Krismasi kwa lugha na tamaduni tofauti. Sr. Sandra Paolacci, Mkubwa wa Jumuiya hiyo, alitukaribisha kwa furaha na Upendo Mkubwa . Baadhi yao walitushukuru kwa furaha kubwa na upendo ambao tuliwapelekea na wakatukaribisha tena kwa mara nyingine. Uwepo wetu umeongeza tumaini na upendo katika maisha yao.



***Sr Rani Padayattil, ASC***

## Kalenda ya Uongozi Mkuu

**3-14 february:** Kuanza kwa Mkutano wa (CGE), Consiglio Generale Esteso (CGE) wenye washiriki wafuatao: Wakuu wa Region, washauri wa Region wanaohusika na malezi na Waratibu wa Foundation.
**4 febbraio:** Sherehe ya Mtakatifu Maria De Mattias na kuanza rasmi kwa Novisiati yenye Wapostulanti saba wa Shirika.
**10 february:** Kufunga maadhimisho ya miaka 185 huko Acuto.



## Siku za kuzaliwa: Tusherehekee Uhai

| | | |
|---|---|---|
| miaka 40 | | |
| **Sr Thi Ha Tran** | 15/02/1980 | Corea |
| miaka 70 | | |
| **Sr Danuta Paterek** | 11/02/1950 | Wrocław |
| **Sr Maria Orsino** | 22/02/1950 | Italia |
| miaka 90 | | |
| **Sr Mary Schoenecker** | 01/02/1930 | USA |

## Waliorudi nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 04/01/2020 | **Sr Ermelinde Kräutler** | Schaan |
| 06/01/2020 | **Sr Evetha Lusiani Ndetembea** | Tanzania |
| 07/01/2020 | **Sr Theresa Marie Braun** | USA |
| 17/01/2020 | **Sr Palma Ciociola** | Italia |
| 23/01/2020 | **Sr Maria Da Paz** | Manaus |
| 25/01/2020 | **Sr Dubravka Bulaja** | Zagabria |
| 26/01/2020 | **Sr Licia Buccolieri** | Italia |

Gazeti la Kimataifa
Waabuduo Damu ya Kristo
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**
*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA
**Mwaka XXII, N. 2, Februari 2020**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Debora Brunetti**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Johanna Rubin*** *- Kijerumani*